**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI CHARYA,**

**S.L,P 72,**

**SHIRATI – RORYA.**

**08 Desemba 2023**

**JINA LA MWANAFUNZI. .......................................................................................**

**S.L.P.......................................**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHARYA ILIYOKO WILAYA YA RORYA, MKOA WA MARA, MWAKA 2024.**

## UTANGULIZI

1.0 Ninayo furaha kukutarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2024. Shule ya sekondari Charya ipo umbali wa kilometa 20 kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Rorya,Tarafa ya Girango, Kata ya Kitembe.

Masomo yataanza rasmi tarehe 08 Januari 2024, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 08 januari 2024 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 23 januari 2024. Atakaechelewa kuripoti kama ilivyoelekezwa Mzazi/Mlezi atachukuliwa hatua za kishreia .

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE YA SHULE

1. Shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi.(Jinsia zote)
2. Suruali mbili (2) rangi nyeusi na damu ya mzee (kwa wavulana), zisizobana (isiwe modo)zenye rinda 2 na pindo chini.
3. Sketi mbili (2) rangi nyeusi na damu ya mzee kitambaa kizito,(wasichana) zishonwe rinda boxi (yaani rinda kubwa 1 mbele na nyuma na pembeni marinda madogomadogo matatu).
   (Ni marufuku mtoto wa kike kuvaa sketi fupi shuleni . Aidha mwanafunzi atakaeshona sketi fupi atarudishwa nyumbani kushona upya).
4. Viatu vya ngozi vyeusi jozi mbili (2) vyenye kamba na visigino vifupi.(Kwa jinsia zote).
5. Soksi nyeupe jozi mbili (2) au zaidi kwa wasichana na soksi nyeusi jozi mbili (2) au zaidi kwa wavulana.
6. Mkanda wa ngozi mweusi saizi ya kati kwa wavulana.

7. Sweta ya kukinga baridi rangi ya bluu yenye alama ya V shingoni.(Kwa jinsia zote).
8. Tisheti rangi ya bluu yenye kola shingoni, (kwa jinsia zote).
9. Hijabu nyeupe kwa wasichana (waislamu tu).

**2.2 SARE ZA MICHEZO KWA WOTE.**

1. Track suit yenye rangi ya **DARK BLUE** ikiwa na mistari meupe kwa jinsia zote ni lazima
2. Fulana moja rangi ya **DARK BLUE** yenye mikono mifupi na mistari meupe kwa jinsia zote ni lazima
3. Stocking soksi rangi ya bluu (soksi jozi mbili (2) za michezo)

**2.3 VIFAA**

1. Daftari kubwa kumi 10 Quire 3 (counter book).
2. Madaftari madogo kumi (10) ya mazoezi .
3. Kamusi ya Kiswahili kwa Kiswahili na ya kiingereza kwa kiingereza (Dictionary).
4. Kalamu ya wino bluu au nyeusi, rula na kalamu ya risasi (penseli).
5. Mkebe wa hesabu.
6. **Ushauri kwako mzazi/mlezi**:Napenda kukushauri kuwa, mnunulie mwanao vitabu viwili (2) kati ya vifuatavyo
    - Mabala The Farmer
    - Hawa The Bus Driver
    - The Magic Garden
    - Kalulu The Hare

**3.0 ZINGATIO**

3.1 Kabla ya kuamua kufika , tafadhali ijulikane wazi kwamba unazingatia mambo yafuatayo:-

a) Tabia yake iwe nzuri kabisa na uioneshe kwa kufuata sheria na taratibu za jumuiya ya shule.
b) Kazi ni Elimu lazima kuifanya na kuipenda, kazi itafanywa kwa bidii na maaarifa.
c) Wajibu mwingine ni kufuta ujinga kwa kujiongezea Elimu kwa kadri ya uwezo wako na kufuata maelekezo ya viongozi, walimu na watumishi wasio walimu.
d) Kwa namna yoyote ile mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu ndani na nje ya shule.

**4.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.**

**4.1** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu **Na. 25** ya mwaka **1978**. Aidha inazingatia nyaraka na miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

a) Heshima kwa wanafunzi, viongozi, wazazi, walezi, wafanyakazi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
c) Kutimiza kwa makini shughuli za jioni

d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazoelekezwa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa shuleni.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali za umma.

**5.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.**

1) Wizi.
2) Uasherati na ushoga.
3) Ubakaji.
4) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
   ‘’Kama vile uvutaji wa bangi, mirungi,marijuana, kubeli, cocaine n.k.”
5) Kupiga au kupigana.
6) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7) Kudharau bendera ya Taifa.
8) Kuoa au kuolewa.
9) Kusababisha au kupata mimba, ndani au nje ya shule.
10) Kutoa mimba.
11) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule.
12) Kukataa adhabu kwa makusudi.
13) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni.
14) Utoro kwa siku 90 mfululizo.
15) Kukashifu au kudharau dini ya mtu mwingine.

**6.0 MAMBO MENGINE MUHIMU**

a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali, Fomu hii itakabidhiwa kwa Makamu Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI CHARYA**

**..................................**

**BRIGITA G. KAIZA**
**MKUU WA SHULE.**
**MAWASILIANO: 0786 580 060**

**FOMU YA KUKIRI KWA MWANAFUNZI**

Mimi ....................................................................kidato cha..................mwaka.................
ninatoka kijiji cha.............................. kata ya ..............................

Nikiwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Charya ninaahidi kuwa ninapokuwa mwanafunzi wa shule hii.

Ninaahidi kuwa sitashiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai na pia kutovunja amani ya shule.

Mimi (mwanafunzi) ....................................................saini ........................ tarehe.............

**KUKIRI KWA MZAZI/MLEZI**

Mimi mzazi wa .......................................................................kutoka kijiji cha......................
Kata ya .......................................... ninaahidi kuwa mwanangu ..........................................

Nimekubali ajiunge na shule ya sekondari Charya  na pia nimesoma na kuelewa sheria na kanuni zote hivyo nitashirikiana na uongozi wa shule katika hatua zote kwa kipindi ambacho mwanangu atakuwepo shuleni.

Mimi ( mzazi/mlezi) ................................................. ................saini.................................

Simu Na. ..............................................................................Tarehe ...............................

**NB: FOMU HII IRUDISHWE SHULENI KWA**

**MKUU WA SHULE**

**SHULE YA SEKONDARI CHARYA**

**S.L.P 72,**

**SHIRATI – RORYA.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENT'S OFFICE – REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**CHARYA SECONDARY STUDENT'S FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

Student's full name.................................................................................................................................

Age .......................................

I kindly request you to examine him/her physically and mentally if he/she is fit or unfit to pursue O-level studies in our school.

Blood-count ..................................................................................................................................

Urine .............................................................................................................................................

Stool .............................................................................................................................................

Venereal – diseases .......................................................................................................................

T. B ...............................................................................................................................................

Ears ...............................................................................................................................................

Eyes ..............................................................................................................................................

Spleen ............................................................................................................................................

Chest .............................................................................................................................................

**ADDITIONAL INFORMATION:**

If any E.g, physical defects (arm or leg impairments, chronic or family diseases) ect

.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................
........................

I certify that he/she is fit/unfit to persue education as stated

Name ......................................................................................................................

Signature .......................................          Station .......................................................

Designation ....................................

Date ................................................          Official stamp.............................................